

MOLA WETU SAMAHANI

- | | | |
|---|--|---|
| <p>1. Kwa jina lake manani,
Subhana Buruhani,
Nipate kaa kitini,
Nandike karatasini,
Haya ninayo wazia.</p> | <p>5. Bora tuwe utiini,
Amrize tufateni,
Tujengizwa peponi,
Tunusurike motoni,
Mwenyewe akijalia.</p> | <p>8. Yailahi tujalieni,
Tuipate samahani,
Tupewe na afueni,
Hali yetu taabani.
Zidi kutuhurumia.</p> |
| <p>2. Arahimu Rahmani,
A'lhayu Qayumuni,
Yako kwake mkononi,
Ardhi na ya mbinguni,
Ngoja nikuhadithia.</p> | <p>6. Huyo ni Mola amini,
Mwingine hawafanani,
Asiye ushirikani,
Hangii usingizini.
Tafadhalini sikia.</p> | <p>9. Yote tuzingatieni,
Sana tuyafikirini,
Tuyahifadhi moyoni,
Na kukinga kifuani.
Yasipate kuachia.</p> |
| <p>3. Hakimu wa Kiyamani,
Dunia na akherani,
Ajua ya Uwanjani,
Na yaliyo mafichoni,
Asiye kupendelea.</p> | <p>7. Jamani sikilizeni,
Wote nawaombeni,
Tusijitie dhambini,
Kujifanya majinuni,
Bure tutaangamia.</p> | <p>10. Kumi nangia ndani,
Nauacha usukani,
Nimefika ukingoni,
Naiomba samahani.
Kama nimekosea.</p> |
| <p>4. Sote tumo amrini,
Nyama nao ikhiwani,
Alitakalo Enzini,
Hana wa kumhini,
Yote yanatimia.</p> | | <p><i>Yusuf M. Kalala
Washington, D.C.
September 19, 2002</i></p> |